I join hands with every single Senator who has contributed to the Statement. It is abhorrent to hear that a hospital has gone without power for any period.

In addition to what Sen. Mandago suggested; there should be a policy in place that gives hospitals and other essential institutions amnesty in this regard. It is shocking that we are even having this debate that there is a hospital in Mombasa or anywhere else in the country that has its electricity disconnected. Electricity gives life to the people who are seeking services in that essential institution. If it is not me, somebody else should heed my cry in this House to bring a policy of this sort.

Thank you, Mr. Speaker, Sir.

**The Speaker** (Hon. Kingi): Sen. Kinyua.

**Sen. Kinyua:** Asante, Bw. Spika, kwa kunipa fursa hii. Nasimama kuunga mkono Taarifa iliyoletwa na Sen. Faki kuhusu ukakatwa kwa umeme katika hospitali ya Mombasa.

Bw. Spika, swali langu ni hili: Je, wagonjwa wanalipa wanapoenda kutibiwa katika hospitali hii ya Mombasa? Kama hawalipi, jibu la swali langu litakuwa tofauti.

Hospitali hizi zetu tunazojadili hapa, mtu akifariki hupelekwa katika chumba cha kuhifadhia maiti. Watu wanapoenda kuchukua mwili, hulipa kiwango fulani cha pesa. Ikiwa wagonjwa hulipa wanapotibiwa na miili inapochukuliwa kutoka chumba cha kuhifadhia maiti katika hospitali hii, pesa hizo huenda wapi?

Nimemsikiliza Sen. Thang'wa akisema kuna hela zinatengwa na Seneti za hospitali za kaunti zote nchini. Kuna pesa za Mombasa, Laikipia na kaunti zingine. Pesa hizi huwa zinaenda wapi? Ninakashifu ule ukataji wa nguvu za umeme na Kampuni ya Nguvu za Umeme Nchini.

Bw. Spika, tujiulize maswali ambayo ni mazito. Wale ambao wanaohusika na msimamizi wa hospitali zetu, kwa nini hawalipi deni au bili ya stima? Ningependa Mwenyekiti aulize kama kulikuwa na notisi na ya siku ngapi kabla ya kukata stima katika hospitali hiyo kwa ajili ya wale wagonjwa walio katika vyumba vya wagonjwa mahututi. Je, kuna maadishi kuhusu notisi iliyotolewa?

Waswahili husema, mgala muue na haki umpe. Leo tutasema stima zisikatwe mahospitalini. Kesho tutasema stima isikatwe katika vituo vya polisi kama vile alivyosema Seneta mwenzangu.

Bw. Spika, Seneti imetenga pesa ambazo zinazoenda katika kaunti zetu. Sisi kama maseneta tunazembea kazini ikiwa hatutahakikisha kuwa walimu wetu wa chekechea wanalipwa mishahara yao, Kampuni ya Nguvu za Umeme Nchini inalipwa madeni yake na huduma nyingine kufanyiwa wananchi.

Nampongeza Sen. Faki kwa kuleta Taarifa hii. Inafaa iwe funzo kwa kaunti zetu zingine ndio magavana wajue wana jukumu la kuhakikisha kila deni limelipwa.

Bw. Spika, ulikuwa gavana wa Kaunti ya Kilifi na unajua vile mgao wa fedha kutoka Serikali Kuu hucheleweshwa. Mashirika ya Serikali yanafaa kujadiliana na hospitali zetu badala ya kukata stima bila notisi. Nakemea Kampuni ya Nguvu za Umeme Nchini sababu huwa na mbio kukata stima ya yule ambaye hajalipa. Hata hivyo, ukitembea nyumba zetu, vyakula vinaoza sababu stima hupotea kila mara. Juzi, Kenya nzima kulikuwa na giza. Hakuna mtu yeyote aliyepata fidia kutoka kwa kampuni hii. Mimi nilikuwa nimelipa deni yangu ya stima yangu. Kwa hiyo, haikuwa makosa yangu ila ya kampuni.

Jokovu langu au kifaa chochote kikiharibika sababu ya nguvu za umeme kupotea, nina haki kulipwa fidia sababu hiyo si shida yangu bali ni ya kampuni ya umeme.

Jambo hili tutalifuatilia mpaka vitongojini ndio tuone ya kwamba tumepata suluhu la kuhudumu. Tukinyamaza na kusema ni watu wa Pwani wanaangamia, kampuni hii itakakata stima Kilifi, Makueni, Nairobi na kaunti zote nchini. Watakapofika Laikipia, hakuna mtu yeyote atakuwepo kusema Laikipia tunamalizwa.

Ninaunga mkono.

**The Speaker** (Hon. Kingi): Sen. Kinyua, naamini kwamba umetumia lugha sanifu ya Kiswahili.

Sen. Mwaruma.

**Sen. Mwaruma:** Asante, Bw. Spika, kwa hii fursa umenipa ili kuunga mkono Taarifa ya Seneta wa Mombasa, Sen. Faki, kuhusu kitendo cha Kampuni ya Nguvu za Umeme Nchini cha kukata stima katika hospitali ya Rufaa ya Mombasa. Ninakikashifu kitendo hicho kwa kinywa kipana kwa sababu ni cha kufa na kupona. Suala la kukata stima katika hospitali ya rufaa Mkoa wa Pwani, ni la kutamausha, kuhuzunisha na ni lazima tulikashifu vilivyo.

Wale walio katika ile hospitali ni wake, waume au watoto wetu. Mtoto wako akiwa katika ile hospitali, akifa unaweza kuzaa mwingine, lakini yule tayari ashakufa. Mke wako akiwa katika hospitali akifa kwa sababu ya ukosefu wa stima, unaweza kumuoa mwanamke mwingine lakini wa kwanza atakuwa ashakufa. Mume wako akiwa hiyo hospitali akifa, unawezaolewa na mtu mwingine, lakini yule mwingine ashakufa tayari.

Bw. Spika, hili swala---

**The Speaker** (Hon. Kingi): Sen. Cherarkey, hoja yako ya nidhamu ni nini?

**Sen. Cherarkey:** Bw. Spika, nimesikia Sen. Mwaruma akisema ati mke akifa, unaeza oa mwingine, ashakum si matusi? Kwani anamaanisha maisha yalipotezwa si muhimu sababu unaeza kuoa na kzaa mtoto mwingine? Hiyo ni heshima?

Kulingana na Ibara ya Katiba, maisha ni muhimu na huanza kutoka kuchukua mimba kwa mama. Maneno yake hayaambatani na Katiba ya Kenya.

Je, huu ni ungwana?

*(Laughter)*

**The Speaker** (Hon. Kingi): Sen. Mwaruma, nataka kwanza ufafanue kauli yako, kama matamshi yako ni kweli vile Sen. Cherarkey alivyonyukuu. Ikiwa ni kweli ndivyo ulivyozungumza, itabidi uyafutilie mbali kwa hotuba yako maanake maisha ya binadamu wote ni sawa. Maisha ya mama au mtoto yote ni sawa. Kumpoteza mke au mtoto ni kupotea maisha. Hakuna maisha mazito au mazuri kushinda mengine.

Pengine, amekunukuu kimakosa. Utatwambia.

**Sen. Mwaruma:** Bw. Spika, ni katika hali ya kukashifu kitendo cha Kampuni ya Umeme Nchini cha kukata stima. Hiki kitendo kinaweza kupelekea maafa na huwezi kupata maisha ya yule mtu ambaye umempoteza. Maisha ya mtoto yakipotea, huwezi pata mtoto mwingine kama yule. Bibi akifa, huwezi kupata bibi mwingine kama yule. Ndio maana ni kitendo cha kukashifu kwa kinywa kipana.

**Sen. (Dr.) Khalwale:** Hoja ya nidhamu, Bw. Spika.

**The Speaker** (Hon. Kingi): Ni nini, Sen. (Dr.) Khalwale?

**Sen. (Dr.) Khalwale:** Bw. Spika, tunamwelewa Mhe. Mwaruma kama mmoja wa viongozi ambao wamezaliwa katika kabila linaloelewa Kiswahili, *the great people of Taita Taveta County*.

Ikiwa kweli alimaanisha kwamba unaweza zaa baada ya mtoto wako kufa, atwaambie. Kama alimaanisha kwamba unaweza oa baada ya mke wako kufa, atwaambie. La sivyo, lazima ayaondoe matamshi yake kwa rekodi ya Seneti. La sivyo, atakuwa ameonyesha madharau kwa Katiba yetu na pia umuhimu wa maisha ya binadamu.

**The Speaker** (Hon. Kingi): Sen. Mwaruma, jieleze. Je, umesema kwamba heri upoteze bibi kwa sababu unaweza kuoa mwingine?

*(Laughter)*

Maanake mimi sikumsikia akizungumza hayo. Kulingana na hoja ya nidhamu, ni kama wamekusikia ukisema hivyo. Jieleze tu ili tuendelee.

**Sen. Mwaruma:** Asante, Bw. Spika. Katika kupinga na kukashifu kitendo cha Kampuni ya Umeme Nchini cha kukata umeme, tunaweza kupoteza maisha. Hilo ni

kweli. Ukipoteza maisha ya baba yako, huwezi kupata baba mwingine kama yeye. Ukipoteza maisha ya mke wako, hayo maisha ya yule mke wako wa kwanza yamepotea. Unaweza ukoa mwingine, lakini yule wa kwanza, ameenda. Hivyo ndivyo nilivyosema.

Ni kauli mbiu kwa sababu ya kutilia mkazo katika kukashifu kitendo cha Kampuni ya Umeme Nchini cha kukata umeme ilihali huduma ya afya katika hospitali, inategemea stima.

**The Speaker** (Hon. Kingi): Sen. Mwaruma, ukipoteza babako halafu mamako aolewe na mwanaume mwingine, si yule ni babako pia?

*(Laughter)*

Kama vile umempoteza mke na ukaoa mke mwingine.

**Sen. Mwaruma:** Bw. Spika, ni katika kukashifu kile kitendo kwa sababu maisha yatapotea.

**The Speaker** (Hon. Kingi): Sawa, endelea tumekuelewa.

**Sen. Mwaruma:** Bw. Spika, hata kama mama yako ataolewa na mume mwingine na upate baba mwingine, yule mzee ashakufa tayari.

Ningependa kujihusisha na matamshi ya Sen. Mandago ya kwamba jambo hili lilitokea kwa sababu ya ukiritimba wa kampuni hii ya umeme. Inafaa tulate Mswada katika Bunge hili ya kuwapa watu wengine haki ya kusambaza umeme. Hili tendo la kampuni hii ni kwa sababu ya ukiritimba; kwamba ni wao peke yao ambao wanasambaza umeme. Kungekuwa na mashirika mengine ambayo wanashindana nao labda hilo tendo halingetokea.

Kwa upande mwingine ni lazima tujiulize swali hili. Je, Serikali ya Kaunti ya Mombasa imejizatiti namna gani kuhakikisha madeni ya kampuni hii yameliipwa?

Ndio maana ninasema ya kwamba hii Taarifa ikipelekwa kwa Kamati ya Afya, ni lazima wadau wote waje, wakiwemo wakurugenzi wa kampuni ya umeme na viongozi wa Kaunti ya Mombasa. Waje watueleze ni kwa nini stima inaweza kukatwa katika taasisi muhimu kama hospitali.

*[The Speaker (Hon. Kingi) left the Chair]*

*[The Temporary Speaker (Sen. Abdul Haji) in the Chair]*

Bw. Spika wa Muda, vile wasemaji wengine wamesema, Hospitali ya Rufaa ya Mombasa inategemewa na kaunti zote za pwani. Hata kuna wagonjwa wanaotoka nchi za nje kuja kutafuta matibabu katika hospitali hii ya Mombasa.

Kwa hivyo, ninaunga mkono. Kamati husika itakapoangalia hii Taarifa, ningependa na mimi nialikwe kama mhusika mkuu kwa sababu watu wangu wa Taita Taveta huenda hospitali hii kwa matibabu. Huenda miongoni mwao kuna watoto wadogo waliozaliwa au wagonjwa walio katika hali mahututi. Wanaweza kupoteza maisha yao kwa sababu ya utepetevu wa utendakazi wa wakurugenzi na wafanyikazi wa kamuni hii.

**Sen. Kinyua:** Hoja ya nidhamu, Bw. Spika wa Muda.

**The Temporary Speaker** (Sen. Abdul Haji): Je, ni hoja ya nidhamu, Sen. Kinyua?

**Sen. Kinyua:** Bw. Spika wa Muda, mwanasheria, Seneta wa Kaunti ya Nandi, alisema maisha huanza wakati wa uzalishaji. Ni vizuri hilo liondolewe katika rekodi zetu. Ninasema hivyo kwa sababu nakala yetu itaonyesha vile na ninajua yeye ni mwanasheria. Anaweza akanukuliwa katika korti ilihali anajua maisha huanza wakati mwanamke amepata mimba.

(*Sen. Cherarkey spoke off record*)

*'Conception'* sio uzalishaji.

**The Temporary Speaker** (Sen. Abdul Haji): Sen. Cherarkey ulisema hivyo?

**Sen. Cherarkey:** Ndio, Bw. Spika wa Muda.

**The Temporary Speaker** (Sen. Abdul Haji): Kama ulisema hivyo, tafadhali futilia mbali kutoka kwa rekodi yetu.

**Sen. Cherarkey:** Bw. Spika wa Muda, ninaomba kuchangia. Sijui neno *'conception'* linasemwa vipi kwa lugha ya Kiswahili. Mwenzangu anazidi kunipoteza anaposema maisha yanaanza wakati wa kutunga mimba. Nilifikiria yanaanza wakati wa *'conception.'* *'Conception'* inamaanisha wakati mwanamume na mwanamke wanapolala pamoja.

Unasemaaje kwa lugha ya Kiswahili kwa sababu mwanamume na mwanamke wanapolala pamoja, basi hapo ndipo maisha yanaanza. Yani *'conception'* ama uzalishaji.

Ukisema kutunga mimba, unajuaaje kuwa mwanamke ameshika mimba wakati huo. Kuna mchakato ambao unahitajika hapo. Iwapo katika Kiwahili sanifu uzalishaji ina maana tofauti, mimi ninaomba neno la Kiswahili lile ambao lina maana ya *'conception.'*

**The Temporary Speaker** (Sen. Abdul Haji): Sen. Cherarkey, ninafikiri ungesema wakati mwanamke amepata mimba, ndio maisha yanaanza.

**Sen. Cherarkey:** Bw. Spika wa Muda, ninafikiri tu ni dakika kadhaa baada ya mwanamke kupata mimba ndio maisha yanaanza.

**The Temporary Speaker** (Sen. Abdul Haji): Sen. (Dr.) Khalwale, what is your point of order?

**Sen. (Dr.) Khalwale:** Bw. Spika wa Muda, huu mjadala ni muhimu kwa sababu yote tunayozungumza hapa yanawekwa katika rekodi. Kwa hivyo, ninaomba ndugu yangu, Sen. Cherarkey, akubali. *'Conception'* ni wakati mbegu ya mwanamume inaungana na ya mwanamke katika nyumba ya uzazi.

**The Temporary Speaker** (Sen. Abdul Haji): Sen. Cherarkey, utarekebisha maneno yako kwanza.

**Sen. Cherarkey:** Bw. Spika wa Muda, ninakubaliana na Seneta wa ndume kutoka Kaunti ya Kakamega, kwamba maisha yanaanza wakati mbegu ya mwanamke na mwanaume zinapokutana.

Kwa heshima kubwa, ninaomba *HANSARD* irekebisha matamshi hayo.

**The Temporary Speaker** (Sen. Abdul Haji): Asante, Seneta.

Sen. Kavindu Muthama, ungependa kuchangia?

**Sen. Kavindu Muthama:** Asante, Bw. Spika wa Muda, kwa kunipa fursa hii kuchangia Taarifa hii ambayo imeletwa na Seneta wa Kaunti ya Mombasa.

Bw. Spika wa Muda, ni tabia mbaya sana kwa kampuni ya umeme kukata stima katika hospitali za kaunti. Ninakumbuka kwamba katika Kaunti ya Machakos, mwaka uliopita, umeme ulikatwa ilhali kulikuwa na wagonjwa waliokuwa kwa *oxygen*.

Nilipigiwa simu nikaambiwa niende huko hospitalini kwani kulikuwa kumeharibika baada ya stima kukatwa kwa muda wa siku mbili. Mama yule aliaga dunia mara tu nilipofika Kaunti ya Machakos. Kabla sijafika hospitalini, nilimpigia *County Executive Committee Member* (CECM) wa Kawi katika Kaunti ya Machakos. Nilimuamurisha kwamba nikifika hapo, nipate stima imewaka hospitalini. Hakika, stima hiyo ilikuwa imekatwa maksudi. Nilipata wamewakisha stima. Hospitali ililipa deni yao na stima ikarudishwa.

Kabla hao watu wa kampuni hii hawajakata umeme, ni vizuri wawe wakiwasiliana na mazimamishi wa kaunti na kuwapa fursa ya kulipa deni ya umeme. Ni kweli kuwa kampuni hii ya umeme haitaendelea kusambaza umeme tu bila malipo lakini ni makosa sana kwao kukata umeme kwa hospitali. Magavana wengine hawaajibiki kulipa deni au bili za stima za hospitali za kaunti zao ili watu wetu wanaendelea kuumia bure katika hospitalini zetu.

Sen. Faki, ninakushukuru kwa kuleta hii Taarifa hii. Niko katika harakati za kuchukua rekodi ya watoto na watu wazima walioaga katika hospitali ya Machakos wakati kampuni hii ya umeme ilikataa stima. Nitaleta Taarifa hapa kwa maana hao watu lazima wafidiwe na kampuni ya umeme. Ni lazima walipwe. Sen. Faki, Seneta wa Kaunti ya Mombasa nakusihi ufanye uchunguzi na kubaini ikiwa maafa yoyote yalitokana na kukatwa kwa huo umeme katika hospitali hiyo ya Mombasa. Ikiwa kuna watu walikufa, lazima walipwe.

Ni lazima watoto waliokuwa kwenye *incubator* waliaga, watu waliokuwa katika kitengo cha *Intensive Care Unit* (ICU), waliokuwa wanafanyiwa *dialysis* na wale ambao walikuwa kwa *oxygen*, lazima waliteseka na wegine kuaga dunia. Watu hao lazima walipwe. *Kenya Power* na magavana lazima waajibike. Ninaomba Sen. Faki unisikilize maana ni wewe umeleta Taarifa hii hapa Seneti. Lazima ufuatilie suala hili kwa kina katika Kaunti ya Mombasa. Pia mimi naahidi kuchunguza suala hili katika Kaunti ya Machakos. Naomba pia maseneta wengine wafuatilie suala hili katika kaunti zao.

Sen. Faki, ni lazima ufuatilie ujue ni watoto wangapi wakifa kutokana na kukatwa kwa umeme; wale walikuwa kwenye *incubator*, kwenye *oxygen*, kwa ICU na wale walikuwa wanafanyiwa *dialysis* ili ulete hiyo hesabu vizuri hapa tunapoendelea na huu mjadala. Kamati itakapowaalika hapa Seneti wahusika wote ni sharti uwe na hesabu kamili. Pia mimi nitaleta hesabu ya watu wote walioathirika katika Kaunti ya Machakos.

Bw. Spika wa Muda, ninaomba watu wote waliohusika, wachukuliwe hatua kali na ile kamati ambayo kauli hii itakabidhiwa itinde haki.

Naomba kaunti zote kuzingatia umeme wa *solar panels* kwa hospitali. Hospitali zingine hazina hata *generator as a backup*. Stima ikienda, *generator* inafaa kuwaka *automatically* ili tuwache kupoteza maisha ya watu wetu. Wanapaswa kutilia maneno haya maanani. Kaunti zetu ziko na pesa kwa hiyo wanaweza kununua *generators* za nguvu na kuweka *solar panels* ili watu wetu waache kupoteza maisha.

Bw. Spika wa Muda, ninaunga mkono hii Taarifa hii na ninakashifu hiki kitendo cha kampuni ya umeme.

**The Temporary Speaker** (Sen. Abdul Haji): Sen. Murgor, please proceed. Tafadhali, keep time.

**Sen. Murgor:** Asante, Bw. Spika wa Muda.

I am very grateful for the opportunity you have given to me to share my thoughts along with my colleagues.

Mr. Temporary Speaker, Sir, you will agree with me and most of those that have faced the power cut in their houses, there is a very reckless and negative attitude from the officers of the Kenya Power (KP). Whenever those officers come, they do not care what your situation is as long as you do not have the money or you have not cleared your bill, they will recklessly mistreat you and never care about requests of any kind.

I believe this comes about because of one company monopolising everything about power. It is my very strong opinion that the nation should find alternative people to provide power so that there is at least some sort of competitiveness in provision and supply of power.

The other thoughts in my observation of these people is the fact that money is driving them crazy such that they do not care whether somebody will die as a result of them disconnecting power or whatever will happen. They have become almost as reckless as the 'matatus' on our roads who just care about money such that they do not think that they are carrying people in their vehicles. It is almost like they have bags of maize in those vehicles.

My other observation is that in that recklessness and carelessness, they do not care about a child who is in an incubator needing that power. The attitude as they go to the hospital such as our colleague Sen. Faki is expressing about in this Statement, is that money driven attitude makes them not care whether there is a child in an incubator or whether there is somebody on oxygen that is really depending on power or any other situation in a hospital or anywhere else.

It is time for us to get an alternative group so that there is competition in provision of power. You can imagine the attitude and the situation of looking for money and not minding about the citizens lighting their houses, streets and so on. They are supposed to be providing power. It is the responsibility of the company that is providing power to light the streets and provide power to be connected into people's homes. It is they who provide that needed commodity.

I believe the attitude in KP should be changed. As a company that is making money, apart from making money, their attitude should also be selling so that there is persuasion and marketing in the process of selling. That means an attitude of seeking the attention and involvement of the consumer.

Mr. Temporary Speaker, Sir, I thank you.

**The Temporary Speaker** (Sen. Abdul Haji): Sen. Cherarkey, you may proceed. You have two minutes, please.

**Sen. Cherarkey:** Bw. Spika wa Muda, utaniruhusu dakika tatu kwa sababu niko na mambo mawili. Kwanza, ninataka kumshukuru, Sen. Faki, wa Kaunti ya Mombasa kwa kuleta Taarifa muhimu. Nilishangaa nilipoona kwenye vyombo ya habari kampuni ya umeme imezima umeme kwa sababu ya mambo kadha wa kadha.

Umeme ni muhimu sana. Ningependa Bunge la Seneti au Kamati husika ihakikishe imetoa makataa kwa kampuni ya umeme. Ikiwa kunaye aliaga dunia kwa sababu ya ukosefu wa umeme katika Hospitali Kuu ya Mombasa mhusika anafaa kuchukuliwa hatua ya kisheria. Mambo kama haya yanaharibu uchumi. Hii ni *economic and health sabotage*.

Hili ni swala la haki za kibinadamu. Kuna watoto waliotegemea umeme huo na pia madawa yalikuwa yanategemea jokofu ili yatumike kwa muda fulani. Kwa hivyo, hii ni hasara kubwa.



Ninauliza kampuni ya umeme katika taifa hili la Kenya iwasiliane na hospitali zetu wanapokata umeme na washirikiane na wasimamizi wa hospitali zile ili tusipoteze maisha.

Nafikiri kampuni ya umeme imepitia changamoto nyingi. Mvua inapokaribia kila wakati umeme unapotea. Tunapata malalamishi ya *transformers* ambazo hazifanyi kazi nchini. Vile vile, hakuna *metres* ambazo wanawekea wananchi kutoka kaunti za Garissa, Mombasa au Nandi kuwezesha nguvu za umeme kuwafikia. Kuna shida kubwa katika usimamzi wa kampuni ya umeme.

Ninaomba Seneti na Kamati husika iwachukulie hatua kali za kisheria na wazipe ridhaa familia ambazo zimepoteza watu wao.

Katika Taarifa hii ya ndugu yetu, ameongeza kuwa kuna utepetevu wa wafanyikazi wa hospitali hio. Kaunti ya Mombasa inayoongozwa na gavana inafaa kuchukuliwa hatua kali. Kwa sababu hakufai kuwa na utepetevu katika utoaji wa huduma za afya hospitalini ya *Coast General Hospital* ambayo ni hospitali kubwa ya rufaa inayohudumia kaunti nyingi katika sehemu za Pwani.

Kwa hivyo, wanafaa kuchukuliwa hatua ili malalamishi haya yakome. Maswala ya afya ni *devolved function* ambayo iko kwa Ratiba ya Nne ya Katiba. Kama kaunti zitashindwa kusimamia maswala ya afya katika taifa la Kenya, itakuwa ni kosa kubwa sana.

Ninaunga mkono na kumshukuru, Sen. Faki. Ikiwezekana, Kamati husika ya maswala ya Afya inafaa kuzuru Kaunti ya Mombasa ili tujue hali ilivyo mbashara. Wanasema vitu kwa *ground* ni tofauti. Kwa hivyo, inabidi Kamati iingilie kati na kushugulikia mambo haya.

Bw. Spika wa Muda, ninashukuru kwa kunipa fursa hii. Ninampa kongole na heko, Sen. Faki.

**The Temporary Speaker** (Sen. Abdul Haji): Asante sana, Sen. Cherarkey. There being no other Senators. There is a Communication from the Chair.

## COMMUNICATION FROM THE CHAIR

### VISITING DELEGATION FROM BUNGOMA COUNTY ASSEMBLY

Hon. Senators, I would like to acknowledge the presence in the Public Gallery of a visiting delegation from Bungoma County Assembly. The delegation comprises eight clerk assistants and two legal officers who are undertaking a training at the Centre for Parliamentary Studies (CPST).

Hon. Senators, on behalf of the Senate and on my own behalf, I extend a warm welcome and wish them a fruitful visit.

Proceed, Senator for Bungoma County.

**Sen. Wafula:** Asante sana, Bw. Spika wa Muda. Nilikuwa nimeketi hapa kama nimetulia tuli nikisikiza na nikaona sura ambazo nazijua. Wamenyonga tai na mabinti wamekula vyema na nyuso zao nyororo kama watu wa Kaunti ya Bungoma.

Ninashukuru sana kuja kwao hapa kwa sababu ugatuzi kuafiki malengo yake ni lazima viongozi katika Bunge la Kaunti la Bungoma na kaunti nzima wajue kuifanya kazi yao na majukumu yanayoambatana na matarajio ya wananchi. Pia, wajumbe wa *ward*

wanapochangia pale mashinani, viongozi hawa ndio huhakikisha maoni na maelezo ya viongozi yanawekwa kwenye vitabu inavyotakikana.

Najivunia uchapa kazi wao. Nimekuwa kule vijijini kwa muda mrefu nikifanya kazi na aliyekuwa Seneta wa Kaunti ya Bungoma. Tulikuwa tunazuru Bunge la Kaunti akiwahudumia au kutoa hotuba za mwaka baada ya mwaka.

Huu ni wakati wangu kuwakaribisha katika Bunge la Seneti na kuhakikisha kupitia, Bw. Spika, na uwezo niliopewa kikatiba na wananchi wa Bungoma kutembea na nyinyi aste kuhakikisha kuwa mnatimiza majukumu yenu pasipo tisho, ubaguzi, au bugdha yeyote.

Ninawakaribisha katika Bunge la Seneti mmejionea kwa macho yenu kwamba mambo yanafanywa sawasawa.

Nitatembea na nyinyi kule nyumbani kuhakikisha kwamba shilingi ya mtozwa ushuru wa Bungoma inafanya kazi. Kupitia Spika wenu, Bw. Situma, mchapakazi mwenzangu, ninajua mko mikononi ya mtu mungwana ambaye si mbadhirifu kama kupe lakini mtu wa moyo mweupe kama pamba.

Karibuni sana watu wangu wa Bungoma. Najivunia nyinyi kuwa hapa. Mungu awabarikie na mjihisi mko katika Bunge ya viongozi ambao wanatajriba ya kisiasa na taaluma mbalimbali ambapo sheria zinatungwa vizuri.

Asante kwa kunitunuku nafasi hii ya kuwakumbatia kupitia kipaza sauti watu wangu wa Kaunti ya Bungoma.

Asanteni na Mungu awabariki.

**The Temporary Speaker** (Sen. Abdul Haji): Proceed, Sen. Cherarkey.

**Sen. Cherarkey:** Thank you, Mr. Temporary Speaker, Sir. I do not want to risk because the Senator for Bungoma County is good in Kiswahili unlike his predecessor, the current Speaker of the National Assembly, who was good in English.

On behalf of the great people of Nandi County, I take this opportunity to welcome the members of the County Assembly of Bungoma. I know they are in the Senate to learn the parliamentary best practices.

I extend a warm welcome to them and state that all the Committees under your guidance and through your office, will facilitate and ensure they are given the necessary support to ensure that when they report back to their work stations, they will be able to discharge their duties with professionalism, ensure it is *mwananchi* centered and be proud of themselves.

I assure them that Members of County Assembly (MCAs) are the first line of defense for the ordinary mwananchi and that is why when there is a problem in the village, the first person the people will go to is their local MCA; be it issues of school fees, development, funerals or any other problems that they face. The first line of defence on the ground is the MCAs. They play the primary oversight role.

In conclusion, it is unfortunate that the country and, especially the Salaries and Remuneration Commission (SRC) continues to look down on MCAs. They are treated with contempt.

The SRC does not want MCAs to be well resourced. It is against the best practices if they are not well-resourced and motivated. If Bungoma County is getting billions of shillings, they can oversight the governor at that level.

MCAs are well resourced to oversight the governor so that when a cattle dip is built, when an Early Childhood Development Education (ECDE) project is being built,

when hospitals and dispensaries are being built, the people and the MCAs of Bungoma are able to do their oversight properly.

The SRC must be called out. I agree on the issue of car grants that the Members of the National Assembly and the Senate are not taxed. Why is the SRC operating in a discriminatory manner by telling them that they must tax their car grant which is against the best practices that we have?

There was a Gazette Notice that was issued by SRC to cut down on their allowances yet these are the people who do a lot of work. I can tell you when you see those MCAs, some of them are earning less than Kshs20,000 or Kshs15,000, but they are able to go around the village for harambees and other activities. We should give them the respect they deserve. These are not the ordinary councillors that were there in the past. These are MCAs with a Speaker, a county assembly, a county government and a county executive.

I want to assure the MCAs of Bungoma that so long as I am still in the House of the Senate and Parliament, I will always champion for the best interests of the MCAs wherever they are. Be it in Bungoma or any of the 47 counties, you can always hear my voice pushing, not only for you to get the best, but to get to serve your people at the lowest level in Bungoma.

Finally, I went to campaign in Kabuchai - I do not know whether the area Senator knows - and I ended up sleeping in Bungoma Police Station during the era of our former President. I slept in Bungoma Police Station. I had campaigned in Kabuchai. I have learned a few lessons.

I want to thank the people of Bungoma because as I was sleeping in Bungoma Police Station, they were gracious enough. They brought me a lot of food, they visited me. So, I will always be grateful to them. I do not know the reason why I was put in a police cell up to date. However, what I appreciate is that they were very hospitable and they visited me.

At that time, the United Democratic Party (UDA) had a candidate for Ford Kenya. We did not know that Ford Kenya would come and join Kenya Kwanza and form the Government. I want to express my gratitude. I travelled around Kabuchai and interacted with those people in Bungoma and I really want to be grateful that the lessons that I picked in Bungoma will remain.

I hope that one day I can go back to Bungoma Police Station and assist in repainting and at least do something there because that was the fourth time in my life whereby I was sleeping while standing. I have been arrested. You know almost all police stations in Nairobi I know them by name and what they look like. That was the only time and I really want to thank them.

Finally, I want to thank them for giving us the Speaker of the National Assembly, your former Senator, hon. Moses Wetangula. We served with him here with distinction.

The Temporary Speaker also served with him when he joined us and also during the beginning of the term. We thank you for giving us Sen. Wetangula. The Presidential vote to be honest was won and lost in Bungoma. You are the people who ensured President William Ruto was elected the fifth President.

Please, pass our regards to the great people of Bungoma that we will work together in Kenya Kwanza. Do not worry about the noise. I heard Sen. Wafula saying

that Ford Kenya will remain an independent Party. Those are in-house issues and we will sit down to iron them.

We value you as members and a family in Kenya Kwanza, I want to assure you from where I stand and knowing the heart and the mind of the President that Bungoma will always remain in a special place in the President's heart. I want to assure you that there are many development agendas that we will push for the benefit of the great people of Bungoma under the Kenya Kwanza Administration.

It is good that you read the signs. If you had stayed in Azimio, you would still be on the roads throwing stones. With those very many remarks, allow me to welcome them and wish them well. We hope we can take tea after this and compare notes.

Congratulations and all the best.

I thank you.

**The Temporary Speaker** (Sen. Abdul Haji): Seneta Mundigi, nimekuona. Unataka kukaribisha wageni?

**Sen. Mundigi:** Bw. Spika wa Muda, ningependa kuwakaribisha MCAs wa Bungoma kwa hiki kikao cha Seneti. Ninawashukuru kwa vile mmekuja kuona ile kazi tunafanya hapa. Hata ukisikia kuna malumbano kidogo, tukiingia kwa hiki kikao huwa tunakuwa kitu kimoja.

Pili, kama kuna watu wanafaa waheshimike ni MCAs kule mashinani. Wakati huu katika Kenya kuna janga la njaa. Yule mtu anaumia kabisa ni MCA. Mara nyingi nimekuwa nikienda nyumbani na yale nimekuwa niyaona kule kutoka siku ya Ijumaa hadi Jumatatu yamefanya nikaanza kuwaonea MCA huruma kwa sababu watu walikuwa wanakuja kwangu wakiwa wengi na mimi ni Seneta.

Niliona ya kwamba katika kila kijiji mtoto akigonjeka lazima MCA akuwe hapo kumhudumia. Katika mambo ya kanisa, MCA yuko hapo. Ni jambo ya ajabu. Ni aibu kubwa sana kwa sababu hata Seneta wengi hawajawahi kwenda kusema asante kwa kanisa na MCAs wamepanga laini. Kama Embu County, wako 30 MCAs na kila wiki wanaenda kusema asante kwa kanisa.

MCA mwenyewe yuko na mambo ya matanga, karo, na kila kitu na unaona ule mshahara anaupata. Kwa hivyo, Seneti ni vizuri tukae chini tutee MCAs waweze kupata hela nyingi kwa sababu ya ile kazi wanafanya kule mashinani.

Pia MCA ndiye anafanya kazi kubwa kuangalia vile gavana anafanya kazi. MCAs huangalia kila kitu, wanapigana kule hata saa ingine wanaambiwa wamekula pesa. Kwa hivyo, mimi niko katika mrengo ya kuunga mkono MCAs waweze kusaidiwa na mambo ya pesa kwa sababu, wanafanya kazi kona zote za kaunti. Kwa hivyo, ningependa kuwapongeza MCAs wote nchini Kenya. Ninaomba Mungu awasaidie mpate hela nyingi.

Asante.

**The Temporary Speaker** (Sen. Abdul Haji): Sen. Wafula, you have a point of order?

**Sen. Wafula:** Kwa hoja ya nidhamu, Bw. Spika wa Muda. Watu wana mbwembwe kuzungumzia mambo ya wajumbe wa wadi. Lakini vijana ambao wako mbele yangu ni wachapa kazi wa Bunge la Kaunti ya Bungoma.

Ijapokuwa tunawatetea MCAs wetu ambao wanatekeleza wajibu ambao unastahili kupewa shukrani, lakini hawa wachapa kazi lazima mambo yao vile vile yaangaziwe katika maeneo yao ya kazi. Kwa mfano, lazima wapandishwe madaraja baada ya muda;

wapewe nafasi ya kuendesha magari ya kifahari; wapewe nafasi ya kupata matibabu katika hospitali na gharama mbali mbali.

Nadhani hawa watu lazima pia mambo yao yaangaliwe. Ama namna gani? Sasa tuko hapo na nyinyi tuhakikishe kwamba MCAs wanapojivunia kuwa MCAs, wachapa kazi katika mabunge 47 nchini Kenya, wao vile vile waweze kupata matunda ya jasho lao na tuongeze pesa katika mabunge haya ili wasimamizi wa Mabunge haya, wapatie vijana wetu nafasi ya kupandishwa mishahara na kujivunia na safari mbalimbali; kufanya utafiti mbalimbali, ili pia wengine wakiomba kazi katika Bunge la Kitaifa mimi nitakuwa tayari kuwashika mkono wakuje hapa wang'are kama hawa wetu wa Seneti na wachape kazi na tujivunie kwamba Bungoma iko na wachapa kazi.

Asante sana, Bw. Spika wa Muda.

**The Temporary Speaker** (Sen. Abdul Haji): Sen. Mariam Omar, what is your intervention?

### QUORUM

**Sen. Mariam Omar:** Thank you, Mr. Temporary Speaker, Sir. I rise pursuant to Standing Order No.34 which states:

“Quorum of the Senate or of a Committee of the Whole Shall be fifteen Members.”

I see that we are few in the House. So, maybe we can ring the bell so that the others will come.

**The Temporary Speaker** (Sen. Abdul Haji): Thank you, Senator.

Clerk, can you confirm the quorum? Clerk, let us ring the quorum bell for five minutes.

*(The Quorum Bell was rung)*

### ADJOURNMENT

**The Temporary Speaker** (Sen. Abdul Haji): Hon. Senators, pursuant to Standing Order No.41, there being no quorum, the Senate stands adjourned until tomorrow, Thursday, 9<sup>th</sup> March, 2023 at 2.30 p.m.

The senate rose at 5.30 p.m.